



NISHATI

HABARI ZA
NISHATI

News **Bulletin**

www.nishati.go.tz [f](#) Wizara ya Nishati [@](#) wizara_ya_nishati_tanzania [@](#) Nishati2017 [Wizara ya Nishati](#)

Toleo Namba 44

Novemba 1 - 30, 2022

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWASHA UMEME WA GRIDI

KASULU, KIGOMA



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akibonyeza Kitufe kuashiria kuzima Majenereta na kuzindua umeme wa Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Kigoma kwenye hafla iliyofanyika Kasulu Mjini tarehe 17 Oktoba, 2022.



**LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA
MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI**

Wasiliana nasi kwa simu namba +255-26-2322018 Nukushi +255-26-2320148 au
Fika Ofisi ya Mawasiliano, Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P 2494, Dodoma

UZINDUZI

EA, KUPOZA NA KUSAMBAZA UMEME
LOVOTI 220/33kV CHA MPOMVU - GEITA

HASSAN
WA TANZANIA

TAREHE:
15 OKTOBA 2022

2



BODI YA UHARIRI

Mwenyekiti

Mhandisi Felchesmi Mramba
Katibu Mkuu

Makamu Mwenyekiti
Kheri Mahimbali

Mhariri

Dorina G. Makaya

Waandishi

Teresia Mhagama
Zuena Msuya
Hafsa Omar
Timotheo Mathayo

Msanifu Kurasa

Lucas Gordon

Wasiliana nasi kwa simu
namba +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148
au

Fika Ofisi ya Mawasiliano
Mitumba Dodoma,
S.L.P 2494, Dodoma



 www.nishati.go.tz

 [Wizara ya Nishati](#)

 [@Nishati2017](#)

 [wizara_ya_nishati_tanzania](#)

 [Wizara ya Nishati](#)



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akibonyeza Kitufe kuashiria kuzima Majenereta na kuzindua umeme wa Gridi ya Taifa kwa Mkoa wa Kigoma kwenye hafla iliyofanyika Kasulu Mjini tarehe 17 Oktoba, 2022.

RAIS SAMIA SULUHU HASSAN AWASHA UMEME WA GRIDI KASULU, KIGOMA

Na Mwandishi Wetu

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu tarehe 17 Oktoba, 2022 kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi, amewasha umeme wa Gridi ya Taifa katika Wilaya ya Kasulu mkoani Kigoma na kuzima mitambo mitatu ya mafuta yenye uwezo wa kuzalisha megawati

3.75 za umeme na kuusambaza kwenye maeneo ya Wilaya ya Kasulu na Buhigwe.

Mitambo hiyo ya mafuta ilikuwa ikigharimu gharama kubwa kuiendesha ambapo Serikali ilikuwa ikitumia shilingi bilioni 13 kwa mwaka na matengenezo ya mitambo ya shilingi bilioni 1 kwa mwaka.

Kwa kuwasha umeme huo wa Gridi, Wilaya

za Kasulu na Buhigwe zimeunganishwa na umeme wa gridi kupitia kwenye kituo kikubwa cha Nyakanazi kupitia Wilaya za Kakonko na Kibondo ambapo kwa sasa umeme unaofika mkoani humo ni wa kutosheleza mahitaji tofauti na hapo awali.

Akizungumza na wananchi, Rais Samia Suluhu Hassan aliwataka wananchi wa Kigoma kuilinda na kuitunza

miundombinu ya umeme iliyopita mkoani humo ili iweze kuwaletea manufaa katika shughuli zao za maendeleo.

Aidha, Rais Samia alisema kwa hivi sasa mkoa wa Kigoma utapata umeme wa moja kwa moja na wa uhakika ambao utavutia wawekezaji mkoani humo na hivyo kukuza uchumi.

RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, SAMIA SULUHU HASSAN AZINDUA VITUO VYA UMEME GEITA

Na Timotheo Mathayo, Geita.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan Jumamosi, 15 Oktoba, 2022 amezindua kituo cha kupokea, kupoza na kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 220/33 kutoka Bulyanhulu hadi Mpomvu Geita.

Kituo hicho kitafanya mkoa wa Geita kupata umeme wa Megawati 90 na Geita pia kuanza kupata umeme wa kutosha kwa shughuli za kiuchumi na za kijamii.

Kutokana na uwepo wa umeme wa kutosha, TANESCO inaweza kuwapelekea umeme

wateja wakubwa na wadogo na tayari Shirika limesaini mkataba na mgodi mkubwa wa Geita Gold Mines (GGM) na kukamilisha njia itakayopeleka umeme kwenye mgodi huo mkubwa.

Mheshimiwa Rais pia amezindua mradi wa kituo cha kupoza umeme cha Mpovu Geita ambapo mradi huo una sehemu tatu ambazo ni Njia ya kusafirisha umeme kutoka Bulyanhulu mpaka Geita yenye uwezo wa kilovoti 220 za umeme. Transfoma zenye uwezo wa kupitisha megawati 90 na usambazaji umeme katika Wilaya ya Geita.

Mkurugenzi

Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande alisema kuwa uzinduzi wa kituo hicho cha Mpomvu utaondoa changamoto iliyokuwepo ya umeme mdogo pamoja na kushindwa kuwapelekea umeme wa uhakika wachimbaji wakubwa na wadogo wa madini.

Akitoa salamu kwa wananchi wa Geita wakati wa Ziara ya Mhe. Rais mkoani Geita, Waziri wa Nishati, January Makamba alisema kuwa jumla ya Vijiji 486 vilivyopo katika Mkoa wa Geita ni vijiji 353 vilivyopata umeme na bado 133 tu ila Serikali imekwisha wapatia wakandarasi kwa ajili ya

shughuli za kuunganisha na kusambaza umeme katika maeneo yaliyobakia.

Alisema kuwa Serikali inaendelea na mipango ya kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji wadogo wa madini, lengo likiwa ni kupunguza matumizi ya jenereta wakati wa shughuli za utafutaji wa madini.

Makamba alisema kuwa Serikali imetenga sh. Bilioni 57 kwa ajili ya kupeleka umeme kwenye migodi ya wachimbaji wadogo na kati ya hizo sh. Bilioni 7 ni fedha kutoka kwa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na Bilioni 50 zimetolewa na TANESCO.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akivuta kitambaa wakati akizindua Kituo cha kupokea, kupoza na kusambaza umeme cha Mpomvu Geita

MANYANYA: TUMERIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA JNHPP

Na Mwandishi Wetu

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa mradi Mkubwa wa Kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere Hydropower Project (JNHPP) ambao unatekelezwa na Serikali kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa nishati ya umeme nchini.

Akizungumza Katika ziara tarehe 15 Oktoba, 2022, Kaimu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mhandisi Stella Manyanya alisema kuwa utekelezaji wa



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ikiwa katika eneo la kuzalishia umeme (Powerhouse) Katika mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP, mara baada ya kutembelea eneo hilo Oktoba 15, 2022.

mradi huo unaenda kasi na kwamba Kamati imeridhika na ujenzi wake ambao kwa sasa umefikia

asilimia 74. “Niseme sisi kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na

Madini tumeridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huu mkubwa, kwani kufikia asilimia 74 za ujenzi ni jambo kubwa, kama mnavyoona hapa hizi transfoma zote 27 zikiwa ni moja ya miundombinu itakayo wekwa kwenye mradi huu wa JNHPP zinaashiria kuwa mradi upo mwishoni”, Alisema Mhandisi Manyanya.

Aidha, Mhandisi Manyanya aliomba Serikali iwe na utaratibu wa kuwatambua vijana ambao wanatekelekeza miradi mikubwa ya kimkakati ili waweze kuendeleza ujuzi wao mahali ambapo wanatakiwa na katika



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ikiangalia Transfoma zitakazotumika Katika mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP, mara baada ya kutembelea mradi huo Oktoba 15, 2022.

MANYANYA: TUMERIDHISHWA NA UTEKELEZAJI WA MRADI WA JNHPP

utekelezaji wa miradi mingine nchini wapate kusaidia kwa ujuzi wao walioupata kutoka katika miradi hii mikubwa ikiwemo, JNHPP, Mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa SGR, Mradi wa ujenzi wa madaraja mbalimbali na meli ambapo kila mradi una vijana wanaopata ujuzi.

Mhandisi Manyanya alisema kuwa mradi huo umetoa ajira zipatazo 13,000 huku ajira 11,800 zikiwa ni kwa wazawa na ajira 1,200 zikiwa kwa Wageni na utagharimu fedha za kitanzania shilingi trilion 6.5 na ukikamilika utaongeza megawati zipatazo 2,115.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi kutoka Shirika la Umeme



Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, ikipata maelezo kutoka kwa Watalaam wa TANESCO waliopo Katika mradi wa kuzalisha umeme wa JNHPP, mara baada ya kutembelea mradi huo Oktoba 15, 2022.

Tanzania (TANESCO), Mhandisi Athanasius Nangali alisema kuwa wapo tayari kutekeleza mradi huo kwa ubora unaotakiwa ili uweze kusaidia kwenye uchumi

wa nchi kama Serikali inavyoelekeza.

“Tutaendelea kufanya kazi usiku na mchana ili tu kuhakikisha kuwa mradi huu unakamilika kwa ufanisi mkubwa,

kwa ubora unaotakiwa na wakati ili tuweze kuzalisha umeme wa kutosha kwa ajili ya kusaidia uchumi wa nchi yetu”, alisema



Sehemu ya mradi wa JNHPP ambapo maji yatapita kwenda kuzalisha umeme (Waterhouse) ikiwa katika hatua za mwisho kukamilika kama inavyoonekana kwenye picha.



Sehemu ya mradi wa JNHPP ambapo maji yatatunzwa kwenda kuzalisha umeme (Main Dam) ikiwa katika hatua za mwisho kukamilika kama inavyoonekana kwenye picha.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti wakiwa katika eneo la gati ya kushushia mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam mara baada ya kufika bandarini hapo kuona jinsi shughuli za ushushaji na upimaji mafuta zinavyofanyika.

KAMATI YA BUNGE YA BAJETI YAKAGUA SHUGHULI ZA UPAKUAJI NA UPIMAJI MAFUTA DAR ES SALAAM

**Na Theresia Mhagama
Dar es Salaam**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti imefanya ziara katika maeneo yanayotumika kupakua mafuta kutoka kwenye Meli na kupima katika Bandari ya Dar es Salaam na Kigamboni mkoani Dar es Salaam.

Ziara hiyo ilifanyika tarehe 13 Oktoba, 2022 ikiwa na lengo la kujihakikishia kuwa kazi

za ushushaji wa mafuta na upimaji mafuta katika sehemu hizo zinafanyika kwa ufanisi na Serikali inapata mapato stahiki.

Baada ya kufanya ukaguzi huo, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mhe. Daniel Sillo, aliipongeza Serikali kwa jinsi ilivyowekeza katika miundombinu ya ushushaji wa mafuta pamoja na mita za kupimia mafuta hayo

ambazo kwa miaka ya nyuma zilikuwa hazipo na hivyo Serikali ilikuwa haipati mapato stahiki.

Alisema kuwa, mita hizo za kupimia mafuta licha ya kuiwezesha Serikali kupata mapato inayostahili, kampuni zinazoagiza mafuta hayo kutoka nje ya nchi pia zinapata uhakika wa kiasi cha mafuta ambacho wamekiagiza.

Vilevile alisema kuwa, Kamati hiyo ilifanya ziara katika Bandari ya

Mtwara ambapo pia Wajumbe walishuhudia juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuiendesha sekta ya mafuta kwa ufanisi kwani mita za kupimia mafuta katika bandari hiyo zinafanya kazi vizuri na pia upanuzi wa bandari pamoja na sehemu za kuhifadha mafuta unaendelea vizuri hali itakayofanya bandari hiyo kupokea mafuta kwa wingi zaidi.



Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Sillo akizungumza jambo wakati Kamati hiyo ikiwa katika sehemu ambayo inaruhusu mafuta kutoka kwenye meli kwenda kwenye sehemu za kuhifadhiya mafuta zinazomilikiwa na kampuni mbalimbali zinazofanya biashara ya mafuta.

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti wakiwa katika eneo la kupima mafuta katika eneo la Kigamboni mkoani Dar es Salaam.



Baadhhi ya miundombinu iliyopo katika eneo lililofungwa mita za kupimia mafuta katika Bandari ya Dar es Salaam.

BYABATO AWATAKA WANANCHI MBARALI KUTOINGIZA MIFUGO KWENYE VYANZO VYA MAJI



Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiongozwa na Mwenyekiti wao Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula (wa tatu kulia) wakiwa katika picha ya pamoja mara baada ya kuwasili Mbarali mkoani Mbeya kwa ajili ya kushughulikia migogoro ya Matumizi ya ardhi. Katikati ni Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato.



Na Godfrey Mwemezi, Mbeya.

Naibu waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amewataka wananchi wa Kata ya Ubaruku Mbarali mkoani Mbeya kutoingiza mifugo kwenye vyanzo vya maji badala yake wavitunze ili visaidie katika upatikanaji wa nishati ya umeme nchini.

Byabato aliyasema hayo tarehe 25 Oktoba, 2022 katika mkutano wa hadhara na wananchi wa eneo la Ubaruku, Mbarali wakati Kamati

Mawaziri wa Wizara za Kisekta wakiongozwa na Mwenyekiti wao Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi Dkt. Angeline Mabula, wakimsikiliza Mkuu wa Mkoa wa Mbeya Mhe. Juma Homera walipokwenda kutazama na kujionea hali halisi ya upungufu wa maji katika mto Ruaha Mkuu.

BYABATO AWATAKA WANANCHI MBARALI KUTOINGIZA MIFUGO KWENYE VYANZO VYA MAJI



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza na wananchi wa Kata ya Ubaruku wakati Kamati ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta walipofanya ziara kwenye eneo la Mto Ruaha Mkuu mkoani Mbeya.

ya Mawaziri Nane wa Wizara za Kisekta walipofanya ziara kwenye eneo la Mto Ruaha Mkuu ambapo Serikali kupitia Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imetangaza kwamba vijiji vitano na vitongoji 41 na sehemu ndogo ya kitongoji cha Magwalisi ambacho kipo kwenye Mamlaka ya Mji mdogo wa Rujewa wilayani Mbarali wananchi wanatakiwa kuhamishwa ili kupisha hifadhi.

Lengo la uamuzi huo wa Serikali ni kutunza na kulinda ardhi oevu na vyanzo vya kupokea na kutunza maji yanayotiririka kutoka mito mbalimbali.

Byabato alisema kuwa, Mto Ruaha ni moja ya mito inayotegemewa kupeleka maji katika bwawa la Mtera na Bwawa la Julius Nyerere hivyo ni vyema ukatunzwa na kuhifadhiwa kwa maslahi mapana ya nchi.

“Tunakubaliana kuwa shughuli zote zinatuhusu sisi wenyewe na sisi Wizara ya Nishati tunayategemea maji hayohayo kuweza kuzalisha umeme, na umeme ukishazalishwa tunautumia kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kwenye viwanda vyetu vinavyochakata mazao mbalimbali hivyo, wanambarali tutunze vyanzo vyetu vya maji”. Alisema Byabato

NAIBU WAZIRI BYABATO ASHIRIKI WIKI YA MAFUTA AFRIKA NA KONGAMANO LA NISHATI RAFIKI NCHINI AFRIKA YA KUSINI



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza katika Wiki ya Mafuta Afrika (Africa Oil Week) na Kongamano la Nishati Rafiki (Green Energy Summit), jijini Cape Town, nchini Afrika Kusini.

Na Mwandishi Wetu

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato ameshiriki katika Wiki ya Mafuta Afrika (Africa Oil Week) na Kongamano la Nishati Rafiki (Green Energy Summit), jijini Cape Town, nchini Afrika Kusini.

Mikutano hiyo ilianza tarehe 03 Oktoba 2022

na kumalizika tarehe 07 Oktoba 2022.

Katika mikutano hiyo masuala mbalimbali yalijadiliwa ikiwemo Mafuta na Gesi Afrika pamoja na Nishati Salama Afrika.

Mikutano hiyo imeandaliwa na Kamisheni ya Nishati Afrika (AFREC), Wiki ya Mafuta Afrika na Kongamano la Nishati Rafiki ambapo viongozi

wa AFREC, Mawaziri, Mashirika ya Mafuta ya Kiserikali, Taasisi Mbalimbali Afrika na Kimataifa na Sekta Binafisi wamehudhuria.

Naibu Waziri Byabato katika mikutano hiyo aliambatana na Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Balozi Ombeni Sefue, Kaimu Kamishna wa Umeme na Nishati Jadidifu, Edward Ishengoma, Katibu Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC) Bi. Beng'i Issa, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Mha. Charles Sangweni na Wataalam kutoka TPDC.



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akizungumza katika Wiki ya Mafuta Afrika (Africa Oil Week) na Kongamano la Nishati Rafiki (Green Energy Summit), jijini Cape Town, nchini Afrika Kusini.

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI YAPONGEZA PBPA KWA KAZI NZURI

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, tarehe 11 Oktoba, 2022, imefanya ziara ya kukagua Miundombinu ya Kupokea na Kuhifadhi Mafuta kwenye Bandari ya Mtwara na kupongeza Wakala wa Uagizaji Mafuta kwa Pamoja (PBPA) kwa kazi nzuri wanayoifanya ambayo inafanya nchi kuwa na uhakika wa uwepo wa mafuta.

Akizungumza baada ya kutembelea eneo la kupokea mafuta katika Bandari ya Mtwara, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mhe. Daniel Sillo alielezea kufurahishwa



Kaimu Meneja wa Bandari ya Mtwara, Novert Kalembo (aliyenyoosha mkono) akiwaonyesha Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, sehemu ya kupokea Mafuta kutoka kwenye Meli kwenda Bandarini. Kulia kwake ni Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta Kwa Pamoja Erasto Mulokozi.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, wakiwa katika ziara ya kukagua Miundombinu ya Kupokea na Kuhifadhi Mafuta kwenye Bandari ya Mtwara tarehe 11 Oktoba, 2022, mkoani Mtwara.

kwake na kazi nzuri zinazofanywa na PBPA kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali zikiwemo Shirika la Viwango Tanzania, Wakala wa Vipimo na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, katika zoezi zima la kuagiza na kupokea Mafuta na kuiepusha nchi na changamoto ya kukosa mafuta kama baadhi ya nchi zilizopatwa na changamoto hiyo kufuatia vita ya Urusi na Ukrain.

Aidha, Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya Kudumu ya Bunge ya

KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI YAPONGEZA PBPA KWA KAZI NZURI



Mita za kisasa za Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) za kupima mafuta wakati wa ushushaji kutoka kwenye meli.

Bajeti, alieleza kuwa Kamati hiyo itaishauri Serikali kuhusu masuala ya ununuzi wa mafuta kwa wafanyabiashara wa Mafuta wa Mtwara kwa lengo la kuifanya Mtwara kuwa kivutio cha uwekezaji kwenye miundombinu ya Mafuta itakayochochea kukua kwa uchumi wa mikoa ya kusini na kuongeza

biashara kwa nchi zinazoweza kupata huduma kupitia bandari ya Mtwara

Amezitaja nchi hizo kuwa ni Msumbiji, Comorro na Malawi.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Wakala wa Uagizaji Mafuta Kwa Pamoja, Erasto Mulokozi alieleza kuwa, hali ya

upatikanaji wa Mafuta nchini kwa sasa ni nzuri.

Alisema, kwa sasa kuna upanuzi umefanyika katika miundombinu ya kuhifadhi mafuta mjini Mtwara ambapo kampuni ya GM imekamilisha ujenzi wa tenki la mafuta lenye uwezo wa kuhifadhi lita milioni 10 na hivyo

kufanya jumla ya hifadhi ya Mafuta katika Bandari ya Mtwara kufikia lita milioni 35.

Alisema uwekezaji huo utaongeza uwezekano wa kuleta Meli yenye mafuta mengi zaidi ikilinganishwa na sasa na hivyo kuleta unafuu wa bei za mafuta kwa mlaji wa mwisho.

Kamati ya Kudumu Bunge ya Nishati na Madini yakagua eneo la mradi wa LNG



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa katika eneo la Likong'o mkoani Lindi ambapo kutatekezwa mradi mkubwa wa kuchakata na kusindika Gesi Asilia (LNG). Anayetoa maelezo kuhusu mradi huo ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania, Dkt. James Mataragio.

Na Theresia Mhagama **Lindi**

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wamekagua eneo la Likong'o mkoani Lindi ambapo kutatekezwa mradi mkubwa wa kuchakata na kusindika

Gesi Asilia (LNG) ikiwa ni sehemu ya ziara ya Kamati hiyo iliyolenga kukagua kazi za uzalishaji wa Gesi Asilia pamoja na miundombinu ikiwemo ya uchakataji na usafirishaji wa Gesi Asilia.

Wakiwa katika eneo hilo, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la

Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Dkt. James Mataragio, aliwaeleza Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa, majadiliano kati ya Serikali na Wawekezaji wa mradi huo yanatarajiwa kukamilika mwezi Disemba mwaka huu.

Alisema kuwa, baada ya kukamilika

kwa majadiliano hayo, kazi za awali katika eneo hilo la Likong'o zinatarajiwa kuanza mwezi Januari mwakani.

Aliongeza kuwa, wananchi waliopisha eneo hilo la mradi tayari wameshalipwa fidia ya shilingi Bilioni 5.6.

Mradi huo wa

Kamati ya Kudumu Bunge ya Nishati na Madini yakagua eneo la mradi wa LNG

kuchakata na kusindika Gesi Asilia iliyogundulika katika Bahari Kuu Kusini mwa Tanzania, utaleta nchini uwekezaji wenye thamani ya Dola za Marekani Bilioni 40, na unatekelezwa na Kampuni ya Shell ya Uholanzi na Equinor ya Norway pamoja na washirika wao.

Wakiwa mkoani Lindi, Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini, walikagua pia miundombinu ya kusafirisha gesi katika eneo la Somangafungu.



Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini wakiwa katika picha pamoja mara baada ya kukagua eneo la Likong'o ambapo kutatekelezwa mradi mkubwa wa kuchakata na kusindika Gesi Asilia (LNG).



Miundombinu ya usafirishaji wa Gesi Asilia iliyopo Somangafungu mkoani Lindi.

Katika eneo hilo la Somangafungu ndipo Gesi Asilia inayochakatwa Madimba mkoani Mtwara na SongoSongo mkoani Lindi zinaingia katika bomba kubwa la inchi 36 ambalo linasafirisha Gesi Asilia hadi Kinyerezi mkoani Dar es Salaam na kutumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo kwenye magari, majumbani, viwandani na kuzalisha umeme.

Kamati ya Kudumu Bunge ya Nishati na Madini yapongeza wazawa kuendesha mitambo ya gesi nchini



Pongezi hizo zilitolewa tarehe 11 Oktoba 2022, baada ya Wajumbe wa Kamati hiyo kufanya ziara katika visima vya gesi katika Kijiji cha Mnazi Bay na Msimbati pamoja na kiwanda cha kuchakata Gesi Asilia katika eneo la Madimba mkoani Mtwara. Ziara hiyo ililenga kujihakikishia kuwa shughuli za uzalishaji gesi pamoja na miundombinu yake inafanya kazi inavyostahiki.

“Kwa mfano kituo hiki cha Madimba ni muhimu sana kwa sekta yetu ya gesi nchini na kinaendeshwa na

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini imeipongeza Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) kwa kuwezesha vijana wa kitanzania kusimamia na kuendesha mitambo ya kuchakata gesi nchini ambayo imewezesha gesi hiyo kusafirishwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kwenye mitambo ya kuzalisha umeme, viwandani, majumbani na kwenye magari.



Kamati ya Kudumu Bunge ya Nishati na Madini yapongeza wazawa kuendesha mitambo ya gesi nchini

watanzania wenyewe katika mfumo mzima wa kuchakata gesi, Tunaipongeza Serikali kwa kuhakikisha kuwa maeneo kama haya yenye uwekezaji mkubwa yanaendeshwa na kumilikiwa na watanzania wenyewe." Alisema Mwenyekiti wa Kamati,

Mhe. Dunstan Kitandula Alisema kuwa, gesi iliyopo inatumika kwa matumizi mbalimbali ikiwemo umeme ambapo zaidi ya asilimia 60 ya umeme nchini unazalishwa kwa kutumia Gesi Asilia na kuongeza kuwa, matumizi ya gesi yameongezeka hivyo



ameiasa Serikali kuvutia uwekezaji zaidi na

kuchimba gesi zaidi ili kukuza uchumi wa nchi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa TPDC, Dkt. James Mataragio, alisema kuwa, mitambo ya kuchakata gesi ya Madimba inachakata gesi futi za ujazo milioni 210 kwa siku ambazo husambazwa kwa bomba kwenda maeneo mbalimbali ikiwemo ya viwanda, majumbani na kwenye mitambo ya umeme.

Alieleza kuwa, matumizi ya Gesi Asilia yanazidi kuongezeka hivyo Shirika hilo limejiandaa kuzalisha gesi zaidi ili kuweza kuwa na gesi ya kutosha kwa ajili ya matumizi mbalimbali.



BYABATO AHUDHURIA MKUTANO WA NGAZI YA JUU WA JOTOARDHI NCHINI EL SALVADOR



Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato akiwa katika Mkutano wa Pili wa Ngazi ya Juu wa Jotoardhi (*2nd High Level Conference of the Global Geothermal Alliance*), uliofanyika tarehe 30 Septemba, 2022 katika mji wa San Salvador, nchini El Salvador.

Na Mwandishi Wetu

Naibu Waziri wa Nishati, Wakili Stephen Byabato amedhuria

Mkutano wa Pili wa Ngazi ya Juu wa Jotoardhi (*2nd High Level Conference of the Global Geothermal Alliance*), uliofanyika tarehe 30 Septemba, 2022 katika mji wa San Salvador, nchini El Salvador.

Mkutano huo ulihusisha Mawaziri,

viongozi wa juu wa Serikali, Wabia wa Maendeleo, Taasisi na Sekta Binafsi.

Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulijadili fursa na changamoto katika

uendelezaji wa Jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme na miradi ya matumizi mengine (direct heat uses) ikitiliwa mkazo katika Sekta ya Kilimo na kuongeza usalama wa chakula.

Mkutano huo uliandaliwa na International Renewable Energy Agency (IRENA), Serikali ya El Salvador kwa kushirikiana na International Geothermal Association (IGA).



Mkutano huo pamoja na mambo mengine, ulijadili fursa na changamoto katika uendelezaji wa Jotoardhi kwa ajili ya kuzalisha umeme na miradi ya matumizi mengine (direct heat uses) ikitiliwa mkazo katika Sekta ya Kilimo na kuongeza usalama wa chakula.

JARIDA HILI LA MTANDAONI HUTOLEWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI, WIZARA YA NISHATI



Fika Ofisi ya Mawasiliano,
Mji Mpya wa Serikali Mtumba, S.L.P. 2494, Dodoma au
Wasiliana nasikwa simu namba: +255-26-2322018
Nukushi: +255-26-2320148